# Ndoto Zilizozambaratika, Ahadi Zisizotimizwa:

## Wasichana Wakimbizi Waliobaleghe katika Kambi ya Wakimbizi ya Kyaka II, Uganda

Utafiti Uliofanywa na Tume ya Wakimbizi ya Wanawake

Machi 2013

*RIPOTI YA WACHANGIAJI WA JAMII*

**SISI NI KINA NANI?**

Tume ya Wakimbizi ya Wanawake (WRC) ni shirika la utafiti na utetezi lilio New York, Marekani. Lengo letu ni kuboresha maisha na kulinda haki za wakimbizi na wanawake, watoto na watu wachanga ambao ni wakimbizi wa ndani. Tunatetea mabadiliko ya sheria, sera na mipango inayoathiri watu walioathiriwa na vita, mashtaka au janga la asili.

**KWA NINI TULIKUJA UGANDA?**

WRC ilisafiri katika Eneo la Kambi ya Wakimbizi la Kyalla II katika Wilaya ya Kyegegwa Kusini mashariki mwa Uganda ili kuzungumza na wasichana wakimbizi waliobaleghe wenye umri wa 10-16. Tulizungumza na wasichana kuhusu matatizo yao na kile ambacho kingeweza kufanywa ili kuboresha maisha yao. Lengo lilikuwa kuhakikisha kuwa uwakala unaofanya kazi na wakambizi unaelewa hali ya kipekee ya wasichana waliobaleghe. Tutatumia matokeo ya utafiti wetu ili kuhimiza uwakala unaofanya kazi na wakimbizi kuandaa mipango inayosaidia kulinda wasichana waliobaleghe.

**TULIFANYA NINI WAKATI WA ZIARA YETU?**

WRC walikutana na wasichana 93 wakimbizi waliobaleghe. Wengi wao kutoka katika Jamuhuri ya Demokrasia ya Kongo; wachache walikuwa wa kutoka Rwanda na Burundi. Pia tulikutana na wavulana wengi waliobaleghe na akina mama 20 na akina baba 25 wa wasichana waliobaleghe. Hatimaye, tulikutana na zaidi ya wafanyakazi 25 kutoka katika uwakala unaofanya kazi katika Kyalla II. Tulizungumza na watu hawa wote kwenye majadaliano ya vikundi maalum na mahojiano ya binafsi. Tuliwauliza jinsi wanavyoona matatizo ya wasichana waliobaleghe na jinsi ambavyo jamii ingeweza kusaidia kuzungumza nao.



Wasichana waliobaleghe katika kikundi cha majadiliano katika Eneo la Bukere, Kyaka II

**MUKTADHA**

Uganda imetia sahihi Mkutano wa 1951 Unaohusiana na Hali ya Wakimbizi na imetia sahihi kwenye Itifaki yake ya 1967. Serikali ya Uganda inaruhusu wakimbizi kuhama na kutafuta ajira ndani au nje ya kambi. Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi (UNHCR), pamoja na NGO nyingi, Afisi ya waziri Mkuu (OPM) ya Serikali ya Uganda na Kamati ya Ustawi wa Wakimbizi (RWC), zinatoa mipango maalum katika afya, elimu, maisha na huduma za usalama. Lakini maisha ya mkimbizi, *haswa msichana mkimbizi,* bado ni magumu sana. Kwa nini?

1. Umaskini ndio sababu kuu ya vurugu, unyanyasaji na utelekezaji wa watoto, haswa wasichana. Wakati mwingine wasichana wanaondolewa shuleni na kulazimishwa kuolewa. Wanafanyishwa kazi nyingi katika sehemu nyingine kwa sababu ya shinikizo la fedha katika familia na kwa sababu hawana namna katika maisha. Wasichana wengi hawatumii huduma zinazopatikana kambini. Wasichana wanapodhulumiwa na vurugu na unyanyasaji wa kingono, huwa nadra sana wao kuripoti kwa sheria. Badala yake, majadiliano ya familia yanafanyika kwanza, ambapo wasichana hawana au wana mamlaka machache ya kusema chochote kuhusu maamuzi yanayoathiri maisha yao yote.
2. Ingawa elimu ya msingi ni ya bila malipo na usajili katika shule za wasichana umeongezeka katika miaka ya hivi karibuni, idadi ya wasichana wanaosalia shuleni ni chache ikilinganishwa na wavulana katika shule zote za kambi (shule za msingi na upili). Kwa sababu familia haziwezi kumudu kununua vifaa muhimu vya shule, kila mara wasichana wanalazimika kuacha shule. Wakati mwingine wasichana hupata mimba au kuozwa mapema, na basi kuacha shule. Hii inaathiri vibaya hatima yao na maisha watakayoishi kama watu wazima.

**TULIJIFUNZA NINI?**

1. Wasichana wanaathirika na utovu wa usalama wa kimwili ndani na nje ya kambi. Njia ndefu za kuenda shuleni, karibu na vyanzo vya maji, shuleni na nje kwenye barabara, wasichana wanadhulumiwa na unyanyasaji wa kimwili na uoga wa kupigwa na marafiki, walimu, wazazi, wanaume na wavulana.
2. Viwango vya kuacha shule kwa wasichana ni vya juu kwa sababu ya umaskini na ukosefu wa pesa za kulipa vifaa msingi, kama vile vifaa vya shule, vitabu na sare. Pia wasichana wako katika hatari ya kuacha shule kwa sababu wanadhulumiwa kingono na vurugu, kupata mimba mapema.
3. Elimu ya msingi inafunzwa katika baadhi ya maeneo katika lugha ya Kitoro Uganda. Kutokana na hayo, watoto wengi hawawezi kusoma ishara kuhusu jinsi ya kuripoti vurugu inayosababishwa na ngono au jinsia ambazo zinachapishwa kote kambini katika Lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hii inaongeza hatari kwa wasichana.
4. Dhuluma ya vurugu na unyanyasaji wa kingono ni sehemu kubwa katika maisha ya msichana. Wasichana huwa ndio wanaodhulumiwa zaidi, lakini pia hawasikizwi. Programu madhubiti za kuzuia na kushughulikia vurugu na unyanyasaji ni chache, na wasichana hawana fursa nyingi za kushirikishwa katika programu hizi zinapokuwepo.
5. Wasichana huofia kuhusu masuala mwngi ya afya, pamoja na kupata mimba mapema, lakini huduma za afya haziwasaidii waliobaleghe au wasichana. Wasichana wanaogopa kutafuta huduma, hasa huduma za afya za uzazi, kwa sababu ya unyanyapaa wa kijamii.
6. Hakuna nafasi nyingi za mafunzo ya ujuzi, na zilizopo ni ghali mno kwa wasichana. Pia wasichana wanakosa fursa za kuendeleza ujuzi wa maisha kwa sababu kila mara wanashughulikia kazi za nyumbani au wako nje kutafuta pesa.
7. Wasichana wana ufikiaji mchache wa kupata marafiki na watu ambao ni mfano mwema wa kuigwa ambao wanaweza kuwategemea mahitaji yanapotokea. Kwa sababu ya ukosefu wa msaada wa marafiki na mlezi, hawawezi kutumia fursa za kuboresha maisha yao.

**TUNAPENDEKEZA NINI?**

**UNHCR instahili:**

- Kuboresha usalama wa kimwili kambini. Inastahili kuweka taa kuelekea na kutoka visimani na kufyeka misitu karibu na visima. Inastahili kuchunguza na kuweka wafanyakazi wa usalama kwenye barabara, ndani na karibu na masoko, shule, maeneo ya maji na maeneo ya kutafuta kuni.
- Kutetea pamoja na serikali ya Uganda na uwakala wa utekelezaji Kiingereza kitumike katika elimu ya shule za msingi katika viwango vyote. Kuhakikisha kuwa walimu

wamehitimu na kuandaliwa kufunza kwa Kiingera. Kuongeza mafunzo kwa walimu ili wadumishe viwango na kutoa motisha ili kuwaweka walimu wazuri.

- Kuchunguza njia za kuongeza ufadhili wa elimu ya upili ili wasichana waweze kuendelea na elimu yao baada ya shule ya msingi.
- Kuzungumza na wasichana waliobaleghe na wazazi wao au walezi wao kuhusu mahitaji, hatari na suluhisho zilizopendekezwa za kuwalinda na kuwawezesha wasichana. Kuhakikisha kuwa sauti zao zinajumishwa katika miundo ya programu.

**Watoa huduma na mashirika ya jamii ya wakimbizi yanastahili:**

- Kuongeza msaada kwa wasichana kuripoti GBV ndani na nje ya shule. Kuunda mfumo wa uwajibikaji shuleni ili walimu na wanafunzi wawe na mipaka wazi. Kuainisha wazi majukumu na uwajibikaji.
- Kuwapa wasichana ufikiaji rahisi katika mafunzo ya ujuzi wa maisha, kufanya maamuzi, kufikiria kwa kina, ujuzi wa kuwasiliana na kujadiliana. Unda programu kwa mchango kutoka katika vikundi mbalimbali vya wasichana (wasichana waliomaliza shule, wasichana walioolewa na wasichana kutoka katika vikundi vingine vilivyotengwa). Kuwasaidia wafanyakazi kupata njia za kurahisisha wasichana kushiriki.
- Kuwekeza katika mitandao ya jamii ya wasichana. Kuwaruhusu wawe na nafasi na muda wa kujenga urafiki na kutapa msaada wa kuheshimiana kutoka kwa marafiki na watu wazima katika jumuiya zao.
- Kuunga mkono programu za mafunzo ya ujuzi kwa wasichana wakubwa waliobaleghe; jumuisha shughuli ambazo ni mbadala kwa ukulima. Kuwahimiza wasichana wakubwa kufanya biashara isiyo ya kitamaduni kwa wanawake, kwa kuwa hizi hulipa zaidi kuliko biashara ya kitamaduni ya wanawake.
- Kukagua njia za sasa za marejeleo ya vurugu inayotokana na ngono au jinsia (SGBV) na kuhakikisha kuwa huduma za program ni rafiki zaidi kwa waliobaleghe. Kufanya kazi kwa karinu na sekta muhimu (k.v., afya, ulinzi, usalama) ili kutambua kesi za GBV zinazowakumba wasichana waliobaleghe na kukahikisha ufuatiliaji wa kutosha. Kufanya utathmini kwa ufanisi wa njia za marejeleo ili kuhakikisha kuwa waliobaleghe wanazitumia.
- Kuwafikia wazazi na walezi ili waweze kuelewa ubaya wa ndoa ya mapema na dhuluma ya kazi na faida za elimu.
- Wakati vifaa visivyo vya chakula vinasambazwa, vipe kipaumbele vifaa vinavyoathiri ulizi wa wasichana. Hizi ni pamoja na sabuni, karai, sodo, mavazi, pamoja na chupi na sare, vifaa vya shule na vifaa vya makao ili kuboresha nyumba.



Ishara zilizochapishwa katika shule ya msingi katika Bujubuli, Kyaka II

**TUTAFANYA NINI SASA?**

Tume ya Wakimbizi Wanawake itashiriki matokeo na mapendekezo haya ili kuboresha hali ya wasichana wakimbizi Uganda. Tunapanga kuendesha mradi mdogo kupitia mshirika wa karibu Kambi ya Wakimbizi ya Kyalla II ili kujaribu kuweka programu katikati kuimarisha usalama wa wasichana.

Unaweza kusoma ripoti yetu kamili na mapendekezo katika Ndoto Zilizambaratika, Ahadi Zisizotimizw: *Wasichana Wakimbizi Waliobaleghe katika Kambi ya Wakimbizi ya Kyalla II, Uganda kwenye* http://wrc.ms/Wles5V. Tafadhali tufahamishe iwapo ripoti hii ilikufaa kupitia info@wrcommission.org.

**Shukrani**

Tunawashukuru wasichana wakimbizi waliobaleghe, wavulana na viongozi wa jamii waliotumia muda na sauti zao katika utafiti huu.

Ripoti hii ilifanikishwa kupitia ufadhili wa pesa wa Wakfu wa Familia wa Frankel na Wakfu wa Oak.

© 2013 Women's Refugee Commission (Tume ya Wanawake Wakimibizi)

WOMEN'S REFUGEE COMMISSION

Women's Refugee Commission (Tume ya Wanawake Wakimbizi)
122 East 42nd Street
New York, NY 10168-1289
212.551.3115
info@wrcommission.org

www.womensrefugeecommission.org